


## HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI



Kumb.Na. S.20/110/VOL.IV/424

Tarehe 05.09.2017

### TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji ana karibisha maombi ya watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi zilizoordheshwa hapa chini

#### 1. MTENDAJI WA MTAI DARAJA LA III (NAFASI 03)

##### a) Sifa za Mwombaji

Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha Nne(IV) au Sita(VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti katika moja wapo ya fani zifuatazo: Utawala,Sheria,Elimu ya Jamii,Usimamizi wa Fedha,Maendeleo ya Jamii,na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo,Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

##### b) Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Mtaa

- Katibu wa Kamati ya Mtaa
- Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa
- Mshauri wa kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa
- Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umaskini katika Mtaa.

- Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

**c) Ngazi ya Mshahara TGS B sawa na Tsh. 390,000 kwa mwezi**

## **2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II( NAFASI 01)**

### **a) Sifa za Mwombaji**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne wenye cheti cha utunzaji kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

### **b) KAZI ZA WASAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II**

Daraja hili ni la mafunzo katika kazi ,hivyo atafanya kazi kwa maelekezo ya Wasidizi wa Kumbukumbu walio juu yake. Kazi atazojifunza na kufanya ni zile zifanywazona Msaidizi wa Kumbukumbu daraja la I kama ifuatavyo:

- Kutafuta kumbukumbu /nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na wasomaji
- Kudhibiti upokeaji,uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
- Kuchambua,kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katikamakundi kulingana na somo husika(Classfication and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi
- Kuweka /kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki(file racks/cabinets) katika masjala/vyumba vya kuhifandhia kumbukumbu.
- Kuweka kumbukumbu(barua,nyaraka nk) katika mafaili
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

**c) Ngazi ya Mshahara TGS B sawa na Tsh. 390,000 kwa mwezi**

### **3. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 02)**

#### **a) Sifa za Mwombaji**

Kuajiriwa wenye Cheti cha Mtihani wa Kidato cha IV, Wenye Leseni daraja la C ya uendeleshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajali, wenye Cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II

#### **b) KAZI ZA KUFANYA**

- Kuendesha magari ya abiria na malori
- Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote , na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- Kufanya matengenezo madogo madogo katika
- Kutunza na kuandika daftari la safari “Log-book” kwa safari zote

#### **c) Ngazi ya Mshahara TGOS A sawa na Tsh. 300,000 kwa mwezi**


#### **MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE**

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania
- Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) pamoja na picha moja ya Passport size za hivi karibuni.
- Kwa urahisi wa mawasiliano waombaji wanashauriwa waonyeshe namba za simu za kuaminika
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya kidato cha nne na sita na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Testimonials, Provisional Results, Statement of results **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji wawe na umri chini ya miaka 45
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni Tarehe 19/09/2017 ( Wiki mbili baada ya Tangazo hili ).  
Maombi yote yatumwe kupitia Anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI  
S.L.P 44  
KIGOMA**

Limetolewa na

  
**B.D. NINALWO  
KAIMU MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA  
KIGOMA/UJIJI**

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
KIGOMA/UJIJI**